# Pumba yaathiri maisha ya mjane

NA VICTOR BARIETY, GEITA

UGUMU wa maisha umewafanya kinamama wengi kuwa wabunifu.

Mkoani Geita, kuna wanawake wanaouza matunda, kufanya vibarua vya kuchota maji kwa ajili ya ujenzi, kukata kuni na mkaa na wengine kupeta na kuuza pumba mashineni.

Mjane Sophia Ismail (51), mkazi wa Mtaa wa Kalangalala, Kata ya Kalangalala, katika Halmashauri ya mji wa Geita, anaendesha maisha yake kwa kupeta na kuuza pumba laini katika mashine ya Ahmed Mbarack, maarufu kwa jina la Msomali. Mashine hiyo inao akina mama 20 wanaojishughulisha na kazi hiyo.

Sophia anasema aliamua kuuza pumba kwa wafugaji wa kuku na nguruwe, kazi ambayo ni hatari kwa afya yake ili kukabiliana na hali ngumu ya maisha.

Anasema tangu Machi 13, 2013, amekuwa akiuza pumba laini ambazo hutumika kutengeneza chakula cha mifugo kama kuku ng'ombe na nguruwe.

"Ninamiliki familia ya watoto 15, ambao wote ni wanafunzi. Sikuwahi kufikiria kama siku moja ningefanya kazi hii, lakini tangu mume wangu Joackim Ismail, afariki Julai 4 mwaka 2011, nilijikuta nikitafuta mbinu za kujikwamua na umaskini na kuepusha wanangu wasiwe ombaomba mitaani.


"Sikubahatika kusoma, niliishia darasa la tano kutokana na mazingira magumu ya kiuchumi waliyokuwa nayo wazazi wangu, hivyo kupata kazi nzuri si jambo rahisi," anasema Sophia.

Akizungumzia namna anavyopata pumba, anasema wafanyabiashara wanapopeleka mpunga mashine kwa ajili kukoboa, yeye anauanika, ukikauka anaukusanya na kuuweka katika magunia kisha anausombea katika kinu cha mashine ili ukobolewe na baada ya hapo malipo yake huwa ni pumba laini.

Anasema licha ya kazi hiyo kuwa ngumu, kwa sasa bei ya pumba imeshuka mno ikilinganishwa na kipindi cha nyuma.

Anasema awali gunia la pumba la debe sita walikuwa wanauza kwa Sh 5,000 na debe moja Sh 1,000; lakini sasa hivi watu hawana fedha hivyo wanalazimika kushusha bei na kuuza gunia moja kwa Sh 3,000.

"Pesa ninayoipata hapa ni kidogo, haikidhi mahitaji yangu lakini sina jinsi. "Vumbi litokanalo na ukoboaji wa nafaka kuanzia alfajiri hadi jioni ninapokuwa mashine huwa linatuathiri mno lakini sina jinsi. "Mara kwa mara huwa naugua mafua na kikohozi hali ambayo inadhoofisha afya yangu," anasema



Sophia Ismail akiandaa pumba kwa ajili ya kwenda kuuza

Sophia na kuongeza:

"Pamoja na madhara yote hayo, kwa mwezi huwa naambulia Sh 70,000 tu."

Anasema siku moja akibahatika kuonana na Rais Dk. John Magufuli, angemwambia awaangalie mno wanawake hususan wajane, maana wana uhitaji mkubwa kuliko wanaume.

# Ulemavu ulivyosababisha atelekezwe na mumewe

NA FLORENCE SANAWA, MTWARA

WAKATI jamii ikiendelea kupinga ukatili wa kijinsia katika maeneo mbalimbali nchini bado unyanyasaji kijinsia umeendela na kuleta madhara makubwa huku wanawake wakiwa ndiyo wahanga wa ukatili huo.

Wako wanawake ambao wamefanyiwa vitendo vya ukatili na waume zao na kufukuzwa hali iliyochangia maisha magumu kwa wanawake hao ambao wengi wao huachwa na watoto.



Shakira Waziri

Shakira Waziri ni miongoni mwa wanawake waliokumbana na visa vya ukatili huo baada ya kutelekezwa na mumewe baada ya kupata ulemavu wa viungo.

Binti huyo ambaye hawezi kuongeza wala kutembea hivi sasa anaishi kwa babu yake Hamis Waziri katika Kata ya Likombe Manispaa ya Mtwara Mikindani.

Shakira ni mjukuu wa kwanza wa Waziri ambaye alichukuliwa na rafiki wa mama yake kuelekea mkoani Dar es salaam kuishi naye.

Akiwa huko shakira alipata mchumba ambapo taratibu za ndoa zilifanyika na akaolewa miaka minne iliyopita.

Waziri anasema ugonjwa uliompata mjukuu wake umewashangaza sana kwa sababu wamejaribu kwenda maeneo mbalimbali lakini matibabu yamekuwa yakikosekana hivyo kuwakatisha tamaa.

"Hali yake inatutia hofu kila siku maana hatuoni akipata ahueni, vipimo havionyeshi kama ana ugonjwa wowote, jambo hili linatuongezea hofu kwakuwa tunashindwa kumsaidia.

"Kila siku Shakira anazidi kuteseka, mume hajui hali ya mgonjwa wala hajawahi kuja kumuona, tunaomba msaada ili mjukuu wangu aweze kupata haki zake za msingi kwakuwa hakupewa talaka," anasema Waziri.

**MATATIZO**

**Hali yake inatutia hofu kila siku maana hatuoni akipata ahueni, vipimo havionyeshi kama ana ugonjwa wowote, jambo hili linatuongezea hofu kwakuwa tunashindwa kumsaidia.**

Naye Christina Abdallah mkazi wa Majengo Gezaulole, anasema mazingira ya familia ya Shakira ni magumu hali ambayo inachangia binti huyo kushindwa kupata huduma nzuri inayostahili hasa ukizingatia kuwa ulemavu wake ni wa kulala tu.

"Siku zote binti huyo amekuwa akiishi kwa shida kwakuwa amekuwa akikaa ndani peke yake kwa muda mrefu huku akikosa msaada wa haraka hasa akiwa na njaa au akitaka kujisaidia kutokana na mama yake mdogo kuwa katika mizunguko ya biashara ili kuweza kupata mahitaji ya kila siku.

"Udhoofu wa mwili wake na ulemavu alionao umesababisha awe sugu mwilini hali ambayo inazidi kuwakatisha tamaa ndugu zake," anasema.

Kwa upande wake mama mdogo wa Shakira, Ashura Waziri anasema kitendo alichokifanya mkwewe ni cha kinyama ambacho hakivumiliki kabisa.

"Wakati binti yetu anaondoka alikuwa mwenye furaha sana lakini leo hii amekuwa bubu, hawezi kutembea wala kufanya kazi yoyote... inauma sana," anasema Ashura.

Mama huyo anasema ugonjwa umemdumaza umemfanya aonekane mlemavu wa muda mrefu huku hali yake ikizidi kuwa dhoofu kila siku jambo ambalo linawapa wakati mgumu kama familia.

Seleman Masoud ni Mwenyekiti Mstaafu wa Majengo Geza Ulole, anasema jamii inapaswa kushirikiana ili kusaidia familia zisizojiweza ambazo zimekuwa zikikumbwa na matatizo kama aliyopata Shakira.

"Shakira aliolewa wala hakuachika, tangu tulivyoanza kuona familia yake ikihangaika hatujawahi kumuona wala kumsikia mumewe. Ukimuangalia vizuri Shakira huna haja ya kupata maelezo, anateseka sana amepooza kila kitu anafanyiwa na ndugu zake," anasema Masoud.